

MSONGAMANO WA MALORI TUNDUMA KUWA HISTORIA



Naibu waziri wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na mawasiliano (sekta ya Ujenzi) Mh. Elias John Kwandikwa wa pili kushoto akisalimiana na mkuu wa wilaya ya Momba Mh. Juma Said Irando baada ya kuwasili katika ofisi za mkuu wa wilaya ya Momba alipokua kwenye ziara ya siku moja mkoani Songwe.

Naibu waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (sekta ya Ujenzi) **Mh. Elias John Kwandikwa** afanya ziara ya siku moja mkoani Songwe na kukagua ujenzi wa Hospitali mpya ya Mji wa Tunduma katika eneo la Mpemba unao endelea hadi sasa.



Naibu waziri wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na mawasiliano (sekta ya Ujenzi) Mh. Elias John Kwandikwa wa pili kushoto akisalimiana na baadhi ya wafanyakazi wa Halmashauri ya mji Tunduma

Kabla ya kwenda kwenye kukagua eneo la ujenzi wa Hospitali hiyo Mh. Elias John Kwandikwa alizungumza na baadhi ya viongozi wa wilaya ya Momba katika ofisi ya mkuu wa wilaya **Mh. Juma Said Irando**.

Kwenye kikao hicho Mh. Kwandikwa alisema:

“Maendeleo ya miundo mbinu yanayo endelea kufanyika katika jiji la Dar-es-salaam ya

natakiwa yaende sambamba na maendeleo ya mji wa Tunduma”

Aliongeza kwa kusema kuwa

“Tunduma ni mpaka unao pitishia mizigo mingi sana kwenda nje ya nchi ikitokea Dar-es-salaam hivyo serikali inahakikisha miundo mbinu inaboreshwa kwa kiwango cha juu ili kukidhi mahitaji ya wanatunduma na wageni kutoka nchi jirani”.



Naibu waziri wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na mawasiliano (sekta ya Ujenzi) Mh. Elias John Kwandikwa watatu kutoka kushoto akionyeshwa mpango mkakati wa kupunguza msongamano wa magari na wataalamu wa TANROADS katika barabara ya TANZAM mjini Tunduma

Katika kutatua adha ya foleni ndani ya Mji wa Tunduma alimukahakikishia mkuu wa wilaya kuwa

“Serikali imejipanga kujenga Barabara ya Mpemba –Mwaka ili kupungunza msongamano wa magari pindi magari ya mizigo yanapo vuka kutoka Tanzania kuelekea nchi jirani kama vile Zambia, Zimbabwe, Congo, n.k”

Pia amewataka Wakala wa majengo ya Serikali (TBA) kuharakisha ujenzi wa Hospitali ya Mji wa Tunduma Haraka na kwa ufanisi ili iweze kupunguza adha ya wagonjwa kusafiri umbali mregu kuapata huduma,

Pia kituo cha Afya kinazidiwa hivyo Ukamilishwaji wa haraka wa Hospitali ya Mji utapunguza msongamano wa wagonjwa katika kituo cha afya Tunduma.



Naibu waziri wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na mawasiliano (sekta ya Ujenzi) Mh. Elias John Kwandikwa wa pili kulia akiagua mradi mkubwa wa ujenzi wa Hospitali ya mji Tunduma unaoendelea katika eneo la Mpemba mjini Tunduma